

JIMBO KATOLIKI LA MOROGORO
ALFAGEMS SECONDARY SCHOOL
P.O.Box 6083 – MOROGORO
Tel. 0732-931605
www.alfagems.com

TARATIBU ZA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA KWA WALIOCHAGULIWA

FOMU YA KUKUBALI MASHARTI YA BWENI

JINA LA MWANAFUNZI FORM

TAMKO LA MWANAFUNZI: Kisha kusoma sheria za shule, nimezikubali kwa moyo. Basi, naahidi kuzizingatia kwa makini muda wote nitakaokuwa bwenini na kwamba nitashirikiana na viongozi wake kwa kupokea malezi watakayonipatia kama mwanafunzi, nisidai mambo ya pekee kwa msingi wa umri, asili, kabila n.k.

.....
(sahihi yako)

TAMKO LA MZAZI/MLEZI: Mimi, , nikiwa mzazi/mlezi wake, nathibitisha kuwa ameelewa na kukubali sheria za shule. Kwa jinsi ninavyomfahamu naamini atawenza kuvishika vilivyo. Isipotokea hivyo, niko tayari kukubali uamuzi wowote ambao uongozi wa shule utachukua juu yake.

Kwa kumuandikisha katika bweni hilo, naomba Kanisa Katoliki linisaidie kumlea mwanangu, ambaye ni mfuasi wa dini ya, madhehebu ya

Naomba aruhusiwe siku ya aende kusali katika kanisa la (au katika msikiti wa). Kwa kumuombea ruhusa nachukua mimi jukumu la matendo yake akiwa nje ya shule siku hiyo.

Wakati wa likizo atakuwa anakwenda

Asipoweza kurudi shulenii siku iliyopangwa au nikitaka ahame bweni, nitatoa taarifa mwenyewe.

Ndugu wa karibu wanaoruhusiwa kumtembelea ni:

- 1)
- 2)
- 3)
- 4)

.....
(sahihi ya mzazi/mlezi)

Anwani

Simu

Tarehe

TARATIBU ZA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA

Ndugu , tunafurahi kukujulisha umepata nafasi ya kujiunga na kidato cha kwanza kwenye shule yetu iliyoko katika manipaa ya Morogoro, kata ya Tungi, mtaa wa Mji Mwema (kati ya Msamvu na Nanenane). Karibu sana!

Hakuna malipo zaidi ya ada ambayo ni:

- (a) Kwa mwanafunzi wa kutwa Tsh. 400,000 kwa mwaka.
- (b) Kwa mwanafunzi wa bweni Tsh. 900,000 kwa mwaka.

Unaruhusiwa kulipa kwa mikupuo minne, yaani Tsh. 100,000, au 225,000 kabla ya kila nusu mhula, lakini bila robo hiyo hutapokewa.

Kwa usalama wa wote unaombwa ulipie benki (akaunti yenyne jina la shule iko MKOMBOZI C.B. ikiwa na namba 00120603517801; iko pia CRDB, namba 01J2077746000, lakini benki hiyo inadai uongeze Tsh. 1,000 kama faida yake) halafu vocha uiletete shulenii.

Shule imekubaliwa pia kuwa wakala wa kampuni za simu kwa ajili ya kutuma pesa kwa urahisi zaidi.

- (a) Namba ya Airtel Money ni 0789-978886 na inatumika kwa mawasiliano na kwa kutuma pesa.
- (b) Kumbe ile ya M-Pesa (0752-452444) ni kwa ajili ya mawasiliano tu, halafu kuna namba ya uwakala kwa ajili ya kutumia pesa (237405).

Masomo yataanza tarehe 3-1-2017. Basi:

(a) Ukitaka kuwa mwanafunzi wa kutwa ufike shulenii tarehe hiyo saa 1:15 asubuhi. Ukichelewa wiki moja kuripoti na kuleta vocha ya benki nafasi yako anaweza akapewa mwingine.

(b) Ukitaka kukaa bweni ufike kabla ya saa 10:00 jioni ya tarehe iliyotangulia mwanzo wa masomo (kwa kuwa nafasi hazitoshii kwa wote, watapewa waliowahi kuleta ofisini mwetu vocha ya benki hata kabla ya tarehe hiyo).

Ukichelewa wiki moja kujisajili kwa malipo, nafasi yako atapewa mtu wa akiba.

Ulete kivuli cha cheti cha kuzaliwa na vitu vilivyoorodheshwa hapa chini:

1. Sare kama ifuatavyo (huruhusiwi kuleta nguo za aina nyininge):

(a) Kwa wasichana:

- (i) Shati jeupe lenye maandishi ya shule
- (ii) Sketi ya rangi ya damu ya mzee (ifikie sentimeta 25 kutoka ardhini)
- (iii) Viatu vyeusi visivyo na visigino virefu
- (iv) Soksi nyeupe zisizo na urembo wowote
- (v) Sweta ya rangi ya damu ya mzee
- (vi) Kwa michezo: tisheti yenyne maandishi ya shule, bukta ya buluu na raba
- (vii) Masista wanaruhusiwa kuvaa sare ya shirika
- (viii) Waislamu, kwa ombi la mzazi/mlezi, wanaweza wakaruhusiwa kuvaa hijabu halisi nyeupe isiyo na pambo mradi wanyoe nywele zote

(b) Kwa wavulana:

- (i) Shati jeupe lenye maandishi ya shule
- (ii) Suruali ya rangi ya damu ya mzee
- (iii) Viatu vyeusi visivyo na visigino virefu
- (iv) Soksi nyeupe zisizo na urembo wowote
- (v) Sweta ya rangi ya damu ya mzee
- (vi) Kwa michezo: tisheti yenyne maandishi ya shule, bukta ya buluu na raba
- (vii) Mabradha wanaruhusiwa kuvaa sare ya shirika.

2. Kwa kukaa bweni:

- (a) Tisheti ya kijani yenyе maandishi ya shule
- (b) Nguo ya kulalia na ya kwenda bafuni
- (c) Mashuka na blanketi
- (d) Chandarua iliyotiwa dawa
- (e) Godoro la futi mbili unusu
- (f) Ndoo
- (g) Sanduku imara na salama
- (h) Tauilo na vifaa vingine vya usafi
- (i) Sahani, bakuli, kikombe na kijiko
- (j) Nauli ya kurudi nyumbani wakati wowote.

N.B. Mashati na tisheti za shule, sketi, suruali, sweta, madaftari, kalamu na vifaa vya hisabati vinapatikana shuleni kwa bei nafuu.